

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +255262963309/13/14

Nukushi: +255 262 963 316

Barua pepe: ps@lands.go.tz

Tovuti: www.lands.go.tz



*Mji wa Serikali, Mtumba,
S. L. P. 2908,
40477 DODOMA.*

TANGAZO LA UUZAJI VIWANJA ENEO LA KITELELA JIJINI DODOMA

Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anautangazia umma kuwa zoezi la upangaji, upimaji na uwekaji wa miundombinu ya barabara katika eneo la Mradi wa Viwanja Kitelela mkoani Dodoma limekamilika.

Mradi upo karibu na eneo unapojengwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Msalato ambapo viwanja vimepangwa kwa matumizi mbalimbali yakiwemo makazi, biashara, makazi na biashara, viwanda, maghala na viwanda vidogo vidogo na makazi ya nyumba zaidi ya moja (Housing Estate).

Viwanja hivyo ni vya ujazo wa juu, kati na chini ambapo vinauzwa kwa kila mita ya mraba kulingana na ukubwa na matumizi ya kiwanja kama ifuatavyo: - Makazi (TZS.9,000), Biashara (TZS.11,000), Makazi na Biashara (TZS.9,500), viwanda vidogo, Maghala na housing estate (TZS.11,000).

Fomu za maombi zitatolewa na kutakiwa kujazwa na kurejeshwa ndani ya muda wa siku saba (7) kuanzia tarehe 15 Oktoba, 2024 katika Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Dodoma kuanzia saa tatu (3:00) asubuhi hadi saa tisa (9.00) alasiri. Fomu hizo zitapaswa kulipiwa kiasi cha shilingi 5,000 ambacho hakitarudishwa na kisha fomu kurejeshwa zikiwa pamoja na nakala ya Kitambulisho cha Taifa au Namba ya NIDA, uthibisho wa malipo ya ada ya maombi na picha za pasipoti baada ya kujazwa taarifa zote muhimu.

Waombaji watakaokubaliwa watapewa namba ya malipo (control number) kwa ajili ya kulipia gharama za umilikishaji na malipo yatatakiwa yafanyike ndani ya siku 30 tangu tarehe ya kutolewa kwa control number.

Tangazo hili pia linapatikana katika tovuti ya wizara ya www.lands.go.tz au kituo cha mawasiliano kwa wateja kupitia namba **0262161610, 0739646885 na 0736665533**.

Imetolewa na:

Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
WIZARA WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
10 Oktoba, 2024